TANGAZO LA SERIKALI Na. 283 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA. 290

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA YA MWAKA 2021

Jina na mwanzo wa Sheria kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya Igunga ya Mwaka 2021.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo:

“ada” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Igunga;

“kibali” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mnada" maana yake ni sehemu ambayo kuna shughuli ya kuuza na kununua bidhaa mbali mbali kwa siku maalumu;

"Mnada wa awali" maana yake ni mnada unaomilikiwa na Halmashauri;

"Mnada wa upili" maana yake ni mnada unaomilikiwa na Serikali Kuu;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

## SEHEMU YA PILI
## UTOZAJI ADA NA USHURU

Utozaji wa ada na ushuru

3.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au

ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

5.- (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada yatalipwa kabla ya kupokea huduma inayotozwa ada chini ya Sheria Ndogo hii.

(4) Ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa kwa wakati na kuzingatia kwamba :-

a) endapo unalipwa kwa tukio, ushuru huo utalipwa kabla ya tukio husika kuanza;
b) endapo unalipwa kwa siku, ushuru huo utalipwa mwanzoni kabla ya shughuli ya siku hiyo kuanza;
c) endapo unalipwa kila mwezi, ushuru huo utalipwa ndani ya siku saba za mwanzo wa mwezi husika;
d) endapo unalipwa kwa mwaka, ushuru huo utalipwa ndani ya siku ishirini na moja za mwanzo wa mwaka husika;
e) endapo unategemea huduma au hesabu za mapato kufanyika, ushuru huo utalipwa ndani ya siku thelathini baada ya huduma au hesabu za mapato kufanyika.

(4) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo

cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

6.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru na atapaswa kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

7.- (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri;

(c) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote aliyekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

8. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Barua, Hati, taarifa zinazoandikwa na Halmashauri

9.- (1) Halmashauri inaweza kuandika barua au hati, au taarifa kwa mtu yeyote kwa lengo kutoa taarifa, wito au maelekezo kuhusiana na jambo lolote kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(2) Barua au hati itakayoandikwa na Halmashuri kwa mtu yeyote itaelekezwa kwa mhusika na itapokelewa na mhusika au mfanyakazi wake au mtu ambaye ameachiwa ofisi au mtu mzima anayeishi nyumbani mwa mhusika;

(3) Mtu atakayepokea barua au hati kutoka Halmashuri atapaswa kusaini sehemu atakayoelekezwa kusaini na mtu atakayemkabidhi barua au hati husika kwa ajili ya kuthibitisha kufikishwa kwa barua au hati iliyopelekwa.

## SEHEMU YA TATU
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

10.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
c) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru;
d) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
e) atakataa amri halali ya Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa au wakala anayetekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii;
f) akishindwa kuweka kumbukumbu za vitabu, hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri;
g) atakataa kupokea au kusaini uthibitisho wa kupokea hati, taarifa au notisi kwa ajili yake au mtu mwingine ambaye anafanya kazi ofisini kwake au anaishi nyumbani kwake;
h) atakwenda kinyume na masharti ya

Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha kwanza atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufililisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA
*(Chini ya Kifungu cha 3(1))*

SEHEMU YA KWANZA
ADA

I. ADA ZA VIBALI VYA UJENZI KATIKA MAENEO YA MIJINI AU SENTA ZA KWENYE KATA

| Na | Aina ya Ujenzi | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya makazi | 20,000/= |
| 2. | Nyumba ya makazi na Biashara | 30,000/= |
| 3. | Nyumba ya Biashara | 50,000/= |
| 4. | Uzio | 20,000/= |
| 5. | Jengo ya ghorofa 1 hadi 2 | 100,000/= |
| 6. | Jengo la ghorofa 3 na kuendelea | 200,000/= |
| 7. | Shule binafsi | 200,000/= |
| 8. | Ghala | 150,000/= |
| 9. | Kituo cha mafuta | 200,000/= |
| 10. | Mnara wa mawasiliano | 1,000,000/= |
| 11. | Ujenzi mwingine ambao haukutajwa | 100,000/= |

II. ADA ZA VIBALI VYA UJENZI WA MAJENGO YA KUDUMU VIJIJINI

| Na. | Aina ya Ujenzi | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya makazi | 20,000/= |
| 2. | Nyumba ya makazi na Biashara | 20,000/= |
| 3. | Nyumba ya Biashara | 40,000/= |
| 4. | Uzio | 10,000/= |
| 5. | Jengo la ghorofa 1 hadi 2 na kuendelea | 100,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Jengo la ghorofa 3 na kuendelea | 200,000/= |
| 7. | Shule binafsi | 200,000/= |
| 8. | Ghala | 100,000/= |
| 9. | Kituo cha mafuta | 150,000/= |
| 10. | Mnara | 1,000,000/= |
| 11. | Ujenzi mwingine ambao haukutajwa | 80,000/= |

III. ADA ZA VIBALI VYA UZIO WA UJENZI NA MAENEO YA BURUDANI

| Na | Aina ya Kibali | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuzingira eneo la ujenzi kwa mwezi | 10,000/= |
| 2. | Kibali cha Uzio wa muda, kila mita nne kwa siku | 2,000/= |

IV. ADA ZA VIBALI VYA KUFANYA UKARABATI

| Na | Aina ya Jengo | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya Makazi | 10,000/= |
| 2. | Nyumba ya makazi na biashara | 20,000/= |
| 3. | Nyumba ya biashara | 30,000/= |
| 4. | Uzio | 10,000/= |
| 5. | Jengo la ghorofa 1 hadi 2 | 70,000/= |
| 6. | Jengo la ghorofa 3 na kuendelea | 120,000/= |
| 7. | Shule binafsi | 120,000/= |
| 8. | Ghala | 100,000/= |
| 9. | Kituo cha mafuta | 130,000/= |
| 10. | Mnara wa mawasiliano | 500,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Jengo jingine ambalo halikutajwa | 70,000/= |

V. ADA ZA VIBALI VYA KUBOMOA MAJENGO YA KUDUMU

| Na. | Aina ya Jengo | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya makazi | 10,000/= |
| 2. | Nyumba ya makazi na biashara | 20,000/= |
| 3. | Nyumba ya biashara | 30,000/= |
| 4. | Uzio | 10,000/= |
| 5. | Jengo la ghorofa 1 hadi 2 | 80,000/= |
| 6. | Jengo la ghorofa 3 na kuendelea | 130,000/= |
| 7. | Shule binafsi | 130,000/= |
| 8. | Ghala | 130,000/= |
| 9. | Kituo cha mafuta | 130,000/= |
| 10. | Mnara wa mawasiliano | 600,000/= |
| 11. | Jengo jingine ambalo halikutajwa | 80,000/= |

VI. ADA YA KUKODI UKUMBI WA HALMASHAURI KWA SIKU

| Na | Aina ya Matumizi | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Kwa ajili ya Semina za Mashirika na Miradi | 100,000/= |
| 2. | Matumizi ya serikali | 00 |
| 3. | Matumizi kwa ajili ya Asasi za kiraia | 100,000/= |
| 4. | Matumizi binafsi | 100,000/= |
| 5. | Matumizi mengine yasiyotajwa | 100,000/= |

VII. ADA YA KUKODI KIZIMBA SOKONI

| Na. | Matumizi | Ada (Tshs) Kwa Mwezi |
|---|---|---|
| 1. | Kuuza matunda na mbogamboga | 10,000/= |
| 2. | Kuuza nafaka na mizizi | 10,000/= |
| 3. | Kuuza mitumba | 10,000/= |
| 4. | Kuuza samaki na nyama | 10,000/= |
| 5. | Mama na baba lishe | 10,000/= |
| 6. | Kuuza mazao, bidhaa na huduma nyngine zisizotajwa | 10,000/= |

VIII. ADA YA KUTUMIA ENEO LA SOKO KWA MUDA

Ushuru wa kukodi sehemu katika eneo la soko kwa muda wa siku zisizozidi saba kwa mfanyabiashara ambaye hakujisajili katika rejista ya wadau wa soko au ambaye eneo analotaka kutumia sio lile alilosajiriwa kulitumia itakuwa shilingi 30,000/=

IX. ADA ZA VIBALI VYA MATANGAZO YA BIASHARA MIKUTANO NA SHEREHE

| Na | Aina ya Kibali | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kutangaza biashara ya bidhaa au huduma za ndani ya nchi kwa siku | 10,000/= |
| 2. | Kibali cha kutangaza biashara ya bidhaa au huduma kutoka nje ya nchi kwa siku | 15,000/= |
| 3. | Matangazo ya biashara ya muda kama yale ya kutumia vitambaa, kwa muda usiozidi siku saba | 15,000/= |
| 4. | Kibali cha Disco kwa siku | 10,000/= |
| 5. | Kibali cha sherehe za harusi, send off, n.k kwa kipindi cha hadi siku saba | 10,000/= |
| 6. | Kibali cha mkutano wa hadhara hadi siku saba | 15,000/= |
| 7. | Kibali cha Mkutano wa hadhara wa kidini | 00 |

X. ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

Ada za ukaguzi wa nyama zitakuwa kama zilivyobainishwa katika Sheria ya Magonjwa ya Wanyama No. 17 ya mwaka 2003

*Tangazo la Serikali Na. 283 (Linaendelea.)*

### XI. ADA ZA LESENI ZA BIASHARA

Ada za Leseni za biashara zitalipwa kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 208

### XII. ADA YA LESENI YA CRASHER

Leseni ya Crasher kwenye maeneo ya migodini kwa mwaka italipiwa shilingi 70,000/=

### XIII. ADA YA KIBALI CHA KUANZISHA KITUO CHA KUOSHA MAGARI

Kibali cha kuanzisha kituo cha kuosha magari kitalipiwa Shilingi 50,000/= kwa maeneo ya mijini au senta za kwenye kata na shilingi 30,000/= kwa maeneo ya vijijini.

### XIV. ADA YA UKAGUZI WA MAZINGIRA

| Na. | Aina ya Mazingira | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Kiwanda | 150,000/= kwa mwaka |
| 2. | Kituo cha mafuta | 150,000/= kwa mwaka |
| 3. | Majengo yenye ghorofa zisizopungua mbili | 150,000/= kwa mwaka |
| 4. | Eneo la kuchimba madini ya ujenzi lisiloanzishwa na Halmashauri | 150,000/= kabla ya kuanza uchimbaji na kila mwaka wa fedha kabla ya kuendelea na uchimbaji |
| 5. | Kituo binafsi cha kunenepesha mifugo | 150,000/= kabla ya kutoa kibali cha kuanzisha kituo na kila mwaka |

### XV. ADA ZA VIBALI VYA KUKUSANYA NA KURUNDIKA MABAKI YA BIDHAA KWA AJILI YA KUCHAKATWA UPYA

| Na. | Aina ya Mabaki | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Chupa za Plastiki na mabaki mengine plastiki | 20,000/= kwa mwaka |
| 2. | Chuma chakavu | 20,000/= kwa mwaka |
| 3. | Mabaki ya Kioo | 20,000/= kwa mwaka |
| 4. | Mabaki mengine | 20,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA PILI

USHURU

I. USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| Na. | Aina ya Mazao | Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya chakula | 2% ya bei ya shambani |
| 2. | Mazao ya Biashara | 3% ya bei ya shambani |

II. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na | Aina ya chombo kwa Uwezo wa Kubeba Mzingo | Ushuru kwa Safari (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Gari ya hadi Tani 3.5 | 3,000/= |
| 2. | Gari ya tani 7 | 7,000/= |
| 3. | Gari ya tani 10 | 10,000/= |
| 4. | Gari ya tani 12 | 12,000/= |
| 5. | Chombo cha uzito mwingine usiotajwa | 1,000/= @ tani |

III. USHURU WA MAUZO YA MARUDIO YA MADINI

Mauzo ya marudio ya madini ya dhahabu na madini mengine kama hayo, yatalipiwa ushuru wa 10% ya bei ya mauzo.

IV. USHURU WA HUDUMA KWA KAMPUNI AU TAASISI ZINAZOUZA BIDHAA AU HUDUMA NA WAFANYABIASHARA BINAFSI

Ushuru wa huduma utakuwa asilimia 0.3% ya mapato ghafi bila kuhusisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya mlaji.

V. USHURU WA UNENEPESHAJI WA MIFUGO NDANI YA SIKU TISINI KWA KILA MFUGO

| Na. | Aina ya Mfugo | Ushuru Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Punda | 2,000/= |
| 3. | Mbuzi/Kondoo | 1,000/= |
| 4. | nguruwe | 1,000/= |

VI. USHURU WA KUNI KWA WASAFIRISHAJI WANAOTUMIA CHOMBO CHENYE UWEZO WA KUBEBA KUANZIA TANI MOJA

| Na. | Aina ya Chombo kwa Uwezo wa kubeba | Ushuru kwa Safari (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Tani moja | 3,000/= |
| 2. | Zaidi ya tani 1 hadi tani 3 | 4,000/= |
| 3. | Zaidi ya tani 3 hadi tani 5 | 5,000/= |
| 4. | Zaidi ya tani 5 hadi tani 7 | 15,000/= |
| 5. | Zaidi ya tani 7 | 25,000/= |

VII. USHURU WA MAEGESHO KWENYE MAENEO YA HALMASHAURI NA MATUMIZI YA STENDI

| Na. | Aina ya chombo kwa Uwezo wa Kubeba Mzingo | Ushuru kwa Siku (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Lori kubwa ya tani 5.1 na kuendelea | 4,000/= |
| 2. | Lori la kati ya tani 3 hadi 5 | 3,000/= |
| 3. | Mabasi ya abiria ya tani 3 na kuendelea | 3,000/= |
| 4. | Ushuru wa stendi kwa mabasi yanayopita | 2,000/= |
| 5. | Gari dogo ya abiria ya hadi tani 3 | 1,000/= |
| 6. | Gari jingine dogo chini ya tani 3 | 1,000/= |
| 7. | Pikipiki (ya miguu miwili au mitatu) | 500/= |
| 8. | Chombo kingine ambacho hakikutajwa | 1,000/= |
| 9. | Mtu yeyote anayeingia stendi kusindikiza, au asiye na tiketi au asiye na kibali maalum cha kutumia stendi. | 200/= |

*Tangazo la Serikali Na. 283 (Linaendelea.)*

VIII.USHURU WA TAKA KWA MWEZI

| Na | Aina ya Chanzo cha Ushuru | Ushuru (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kuishi kwa kila kaya yenye mtu 1 hadi 3 | 2,000/= |
| 2. | Nyumba ya kuishi kwa kila kaya yenye watu 4 hadi 6 | 3,000/= |
| 3. | Nyumba ya kuishi kwa kila kaya yenye watu 7 na kuendelea | 4,000/= |
| 4. | Ofisi ya Taasisi au Asasi | 5,000/= |
| 5. | Duka la Biashara ya Jumla | 5,000/= |
| 6. | Washonaji wa nguo kwa cherehani | 1,000/= |
| 7. | Mama au baba lishe | 2,000/= |
| 8. | Duka lolote la rejareja, la bidhaa au huduma, lenye au linalostahili kuwa na leseni ya Biashara | 5,000/= |
| 9. | Kioski au duka dogo | 3,000/= |
| 10. | Saluni | 3,000/= |
| 11. | Duka la kuuza nyama na au samaki | 3,000/= |
| 12. | Duka la kuuza magari | 10,000/= |
| 13. | Duka la Dawa za binadamu au wanyama au mimea | 5,000/= |
| 14. | Ghala | 10,000/= |
| 15. | mgahawa | 5,000/= |
| 16. | Baa | 10,000/= |
| 17. | hotel | 10,000/= |
| 18. | Nyumba ya kulala wageni | 10,000/= |
| 19. | Klabu ya usiku | 10,000/= |
| 20. | Kumbi za sherehe | 10,000/= |
| 21. | Zahanati (taka salama) | 5,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 283 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 22. | Kituo cha Afya (taka salama | 10,000/= |
| 23. | Hospital (taka salama) | 15,000/= |
| 24. | Hospital ya Rufaa (taka salama) | 20,000/= |
| 25. | Kiwanda cha kuzalisha au kuuza mbao kwa taka ambazo sio mabaki ya mbao | 10,000/= |
| 26. | Stoo ya Mkaa | 2,000/= |
| 27. | Dobi | 2,000/= |
| 28. | Wasindikaji wadogo wa mazao | 5,000/= |
| 29. | Wasindikaji wakubwa wa mazao | 10,000/= |
| 30. | Kiwanda kingine kidogo | 5,000/= |
| 31. | Kiwanda kingine cha kati | 10,000/= |
| 32. | Kiwanda kingine kikubwa | 20,000/= |
| 33. | Kiwanda cha kukoboa mpunga, taka ambazo sio pumba | 10,000/= |
| 34. | Shule binafsi ya kutwa | 5,000/= |
| 35. | Shule binafsi ya Bweni | 10,000/= |
| 36. | Kituo cha kuuza mafuta | 10,000/= |
| 37. | Vituo vya kuoshea magari | 10,000/= |
| 38. | Wauza matunda na mbogamboga | 1,000/= |
| 39. | Maeneo ya taasisi na asasi za kiraia | 3,000/= |
| 40. | Wavundika ndizi na wenye vifungashio vya majani | 5,000/= |
| 41. | Kituo cha michezo au mazoezi | 5,000/= |
| 42. | Kilabu ya pombe ya asili | 10,000/= |
| 43. | Karakana | 5,000/= |
| 44. | Fundi viatu | 1,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 45. | Kituo cha mafuta | 8,000/= |
| 46. | Kituo cha kubeti | 5,000/= |
| 47. | Kituo cha kulelea watoto na wenye mahitaji maalum | 0 |
| 48. | Chanzo kingine ambacho hakikutajwa | 3,000/= |

IX. USHURU WA KUTUMIA DAMPO KWA SAFARI MOJA

| Na. | Aina ya chombo kwa Uwezo Wake wa Kubeba Mzigo | Ushuru (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Gari lenye uwezo wa kubeba tani 0 -3.5 | 5,000/= |
| 2. | Gari lenye uwezo wa kubeba tani 3.6 - 5 | 7,000/= |
| 3. | Gari lenye uwezo wa kubeba tani 5.1 - 7 | 10,000/= |
| 4. | Gari lenye uwezo wa kubeba tani 7.1 - 10 | 15,000/= |
| 5. | Gari lenye uwezo wa kubeba tani 10.1 na zaidi | 20,000/= |
| 6. | Chombo kingine ambacho hakikutajwa | 10,000/= |

X. USHURU WA KUSHUSHA MIZIGO SOKONI KWA CHOMBO

| Na. | Uwezo Wake wa Kubeba Mzigo | Ushuru (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Tani 1 | 2,000/= |
| 2. | Tani 1.5 | 2,500/= |
| 3. | Tani 2 | 3,000/= |
| 4. | Tani 3 | 5,000/= |
| 5. | Tani 4 | 6,000/= |
| 6. | Tani 5 | 10,000/= |
| 7. | Tani 7 | 12,000/= |
| 8. | Tani 8 – 10 | 15.000/= |
| 9. | Zaidi ya Tani 10 | 20,000/= |

XI. USHURU WA BIDHAA ZILETWAZO SOKONI

| Na. | Uzito | Ushuru |
|---|---|---|
| A. | Kuanzia kilo 50 hadi 100 | |
| 1. | Vitunguu | 1,000/= |
| 2. | Viazi mbatata | 1,000/= |
| 3. | Karanga | 1,000/= |
| 4. | Nazi | 1,000/= |
| 5. | Mazao mengine | 1,000/= |
| B. | Ushuru wa matenga/boksi | |
| 1. | Maembe | 1,000/= |
| 2. | Papai | 500/= |
| 3. | Nyanya | 500/= |
| 4. | Ndizi | 500/= |
| 5. | Samaki wakavu | 1,000/= |
| 6. | Mabungo | 1,000/= |
| 7. | Samaki wabichi | 1,000/= |
| 8. | Mazao mengine | 1,000/= |
| C. | Ushuru wa viroba (kg 50) | |
| 1. | Nyanya chungu | 500/= |
| 2. | Pilipili | 500/= |
| 3. | Karoti | 500/= |
| 4. | Matango | 500/= |
| 5. | Ndimu | 500/= |
| 6. | Limau | 500/= |
| 7. | Pensheni | 500/= |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Parachichi | 500/= |
| 9. | Peasi | 500/= |
| 10. | Embe | 500/= |
| 11. | Machungwa | 500/= |
| 12. | Viazi vitamu | 500/= |
| 13. | Mihogo | 500/= |
| 14. | Kunde | 500/= |
| 15. | Njegere | 500/= |
| 16. | Hoho | 500/= |
| 17. | Mazao mengine | 500/= |
| D. | Ushuru wa mazao ya nyuki | |
| 1. | Asali kwa kilo | 200/= |
| 2. | Nta kilo | 200/= |

XII. USHURU WA MIFUGO INAYOUZWA MNADANI

| Na. | Aina ya Mifugo | Ushuru Katika Mnada wa Awali | Ushuru Katika Mnada wa Upili |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuku na jamii nyingine ya ndege kwa tenga kubwa | 5,000/= | 5,000/= |
| 2. | Kuku na jamii nyingine ya ndege kwa tenga la kati | 3,000/= | 3,000/= |
| 3. | Kuku na jamii nyingine ya ndege kwa tenga dogo | 1,000/= | 1,000/= |
| 4. | Kila ng'ombe, Punda, ngamia, au farasi | 4,000/= | 1,000/= |
| 5. | Kila Mbuzi, Kondoo au nguruwe | 1,000/= | 500/= |
| 6. | Kila mfugo mwingine usiotajwa | 2,000/= | 1,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 283 (Linaendelea.)*

XIII.USHURU WA KILA SIKU WA SOKO, GULIO NA MNADA KWA WASIOKUWA NA VITAMBULISHO MAALUM VYA WAJASIRIAMALI WADOGO

| Na. | Aina ya Biashara | Ushuru (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Matunda na mbogamboga | 500/= |
| 2. | Nafaka | 500/= |
| 3. | Mitumba | 500/= |
| 4. | Mavazi mapya | 500/= |
| 5. | Fundi cherehani | 500/= |
| 6. | Vyombo vya ndani | 500/= |
| 7. | Dawa za asili | 500/= |
| 8. | Kuku, bata n.k | 500/= |
| 9. | Samaki na nyama | 500/= |
| 10. | Shughuli za mama na baba lishe | 500/= |
| 11. | Huduma za mitandao | 500/= |
| 12. | Vifaa vya kielekitroniki | 500/= |
| 13. | Kuuza mazao, bidhaa na huduma nyingine zisizotajwa | 500/= |

XIV. USHURU WA ZANA ZA KILIMO ZINAZOTUMIKA KIBIASHARA

| Na. | Aina ya Zana na Matumizi | Ushuru(Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Power tiller na Trekta zinazofanyabiashara ya kusomba mazao na mizigo mingine | 3,000/= kwa safari |
| 2. | Mitambo ya kuvuna mazao (Combine harvestor) inayofanya kazi kibiashara | 500,000/= kwa msimu wa mavuno |

JEDWALI LA PILI

(Limetungwa chini ya kifungu cha 11)

KUFILILISHA KOSA

Mimi…………………………………..…………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya mwaka 2021.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini………………………………………Tarehe……………………………………

Nembo na Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga vimebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika 3//4/2020 na ubandikaji huo kushuhudiwa na:-

REVOCATUS L. K. KUULI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Igunga*

PETER ONESMO MALODA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Igunga*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
22 Februari, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*